

Alama Za Kusimama Katika Msahafu

Alama za kusimama zimewekwa na wataalamu wa fani ya Tajwiyd kwa lengo la kuweza kumpelekea msomaji kufikia kutambua mahali panaporuhusiwa na palipokatazwa kusimama. Alama hizi si katika jumla ya maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى), bali ni istilahi zilizokubalika kutumika na ni zenye kueleweka baina ya maquraa na wanafunzi wa Tajwiyd .

Hukmu	Alama
Inaruhusiwa kuendelea lakini kusimama ni vizuri zaidi.	قل
Lazima kusimama	م
Inaruhusiwa kufanya upendavyo, ima kusimama au kuendelea	ج
Inaruhusiwa kusimama ila kuunganisha ni vizuri zaidi	ط
Hairuhusiwi kusimama. Ukisimama kwa dharura rudia maneno ya nyuma uwasilishe	لا
Lazima usimame sehemu mojawapo	❦ ❦
Kipumziko cha haraka mbili bila ya kuteremsha pumzi ¹	س

¹ Rejea mlango wa 'As-Sakt'